JUMAMOSI - MCHANA

Siku ya Jumamosi ilianza kwa heka heka za sherehe za Muungano kama ilivyotarajiwa. Saa moja kamili mimi na mume wangu tulikuwa tayari njiani kuelekea uwanja wa Uhuru ambako sherehe hizo zilikuwa zimepangwa kufanyika kitaifa. Asubuhi yenyewe ilikuwa ni ya joto sana, tena lile joto linalokufanya uamke ukiwa umeloa jasho. Baridi la ndani ya gari lilikuwa ni afueni tosha. Mimi na mume wangu tulikuwa tumeketi kiti cha nyuma na dereva tu tukiwa tumetanguliwa na gari moja la Polisi likiongoza msafara wetu na nyuma kulikuwa na gari jingine. Siku ya Muungano kama zilivyo sherehe nyingine za kitaifa mawaziri kamili hupewa ulinzi maalum na msafara ili kuhakikisha wanaweza kushiriki shughuli muhimu ya kitaifa na kuzuia jambo lolote baya kuweza kutokea.

Mume wangu alikuwa amevalia suti ya rangi ya kijivu isiyokolea sana, shati jeupe na juu yake akiwa amevaa tai ya rangi ya fedha iliyokolea ikiwa imetengenezwa kwa kitambaa king'aacho cha hariri. Kwenye upande wa kushoto karibu na bega lake alikuwa amevaa pini ya bendera ya taifa. Alivaa miwani iliyomfanya aonekane kama mhadhiri wa chuo kikuu kimoja nchini au daktari fulani bingwa. Nilimuangalia kwa chabo na moyoni nilimpenda na wakati huo huo kusikitika. Nilimpenda kwa sababu katika utulivu na ukimya wake hapo alikuwa ni mume wangu, mpenzi wangu wa muda mrefu, rafiki na baba wa watoto wangu. Nilisikitika kwa sababu isingekuwa mambo yake yeye au kitendo alichokifanya na kusababisha mpasuko katika ndoa yetu nisingefikia kujiachia mbele ya Mjamaika au kupanga nilichokuwa nimepanga kufanya Jumamosi hiyo.

Na kwa hakika nisingetumia muda wangu wa jioni ya jana kujinyoa kama kondoo wa sufu! *Maskini mume wangu.*

"Sasa umeamua vipi hunny" aliacha kuangalia nje ya gari na kunigeukia akinirushia tabasamu la huzuni. Nikajifanya 'sintofahamu'

"Kuhusu nini" nilimuuliza kwa upole tu. Dereva macho yake yalikuwa mbele na alikuwa kimya wala hakuonesha dalili kuwa alikuwa anasikia mazungumzo yetu au kuyafuatilia. Amekuwa karibu yetu na familia kwa miaka karibu kumi, hivyo tulishazoea kuzungumza mipango au mambo yetu mbele yake.

"Utakuja nami kwenye tafrija ya Muungano Ikulu? " alisema kunikumbusha. Nilikuwa nakumbuka kuna tafrija ikulu kwani kila mwaka utaratibu ni huo huo wa Rais kuandaa tafrija kwa viongozi wengine wa kitaifa na mabalozi. Lakini nilikuwa na mipango *yangu.* Hata Rais asingeweza kuibadili hata kama angepiga magoti na kulia kwa kunibembeleza.

"Nilikuambia leo pia kuna harusi ya mtoto wa Prof. Rutamuya na tulikubaliana miye niende huko" nilimkumbusha. Huo ulikuwa ni mpango wetu wa awali na nina uhakika alikuwa ameshasahau. Ilikuwa ni hii harusi ndiyo niliyopanga kuitumia kama kivuli cha mpango wangu jioni hiyo.

"Duh, nilishasahau kabisa!" alisema huku akijishika kichwa kujikuna kuonesha masikitiko ya kusahau kitu muhimu. Nikaona na mimi nigongelee msumari kabisa.

“I can’t believe this, yaani ulisahau harusi ya mtoto wa rafiki yako” nilizungumza kwa kuonesha kama kukerwa kwa namna fulani hivi.

“Jamani, na mimi si mwanadamu naweza kusahau” alisema kwa sauti ya hasira kidogo na kama asingekuwepo dereva nina uhakika angepaza sauti na kuwa mkali kidogo. Kwa sekunde chache nilishikwa na ukimya.

Milio ya magari yanayoelekea Kibaha na mikoani yakitupita ulikuwa kama CD iliyokwama kwenye mashine. Pembezoni mwa barabara wananchi walikuwa wameamka na kuanza shughuli zao za kila siku kwa siku hiyo ya Jumamosi; wenye kupanga vibanda vyao vya magenge walikuwa bize kuvipanga na wenye kusubiri madaladala walikuwa wamerundikana kwenye vituo vya mabasi wakingojea madaladala wanayoyataka huku wenye kuendesha baskeli au wenye kutembea kwa miguu nao walikuwa katika mwelekeo huo wa usawa wa mihangaiko. Niliweza kuwaona wavuta mikokoteni nao wakianza taratibu pembezoni mwa barabara hiyo kujivuta taratibu kuelekea maeneo ya stendi kuu ya mabasi ya mikoani pale Ubungo.

“Basi tuyamalize, nitafikisha salamu zako” nilimuambia kwa sauti ya upole. Hakujibu kitu. Alikuwa mwenye mawazo na sikutaka hata chembe kujaribu kuingia kwenye mawazo yake; niliweza tu kuhisi alikuwa *anawaza* nini. Msafara ukanoga kuelekea Uwanja wa uhuru. Nilikuwa nimevaa miwani ya rangi nyeusi kuzuia mwangaza mkali wa jua.

Uwanja wa uhuru ulikuwa umefurika kwa wananchi waliokuwa wamejazana kila upande wengi wao wakiwa wameshikilia vibendera vidogo vidogo vya taifa wakivipepea. Kila kona ya uwanja rangi za bendera ya taifa zilionekana kama maua kwenye shamba kubwa - kuanzia mavazi, vitambaa vya kichwani, kofia na vipepeo vya kujipunga na upepo. Tuliingia mapema hapo baada ya mawaziri wengine wawili. Waziri alipotambulishwa kuwa ndiye ameingia wakati huo sehemu ya kubwa ya jukwaa ililipuka kwa furaha. Waziri amekuwa kwa muda mrefu ni mtu maarufu kwa Watanzania wengi. Alinishika mkono akiniongoza kuelekea nyuma ya jukwaa kuu ambako mawaziri wengine na familia zao walikuwa wameketi. Alipunga mkono kuwasalimia viongozi wengine waliokuwa tayari kwenye jukwaa. Tulioneshwa mahali petu pa kuketi. Nyuma yetu walikuwa wameketi mabalozi na wawakilishi wa taasisi mbalimbali za kimataifa na wageni wengine mashuhuri.

Mimi mwenyewe nilikuwa nimevaa vazi la kitenge la vipande vinne vinavyofanana; sketi ndefu iliyofika hadi miguuni, blauzi iliyokuwa imenyanyuliwa mabegani, kitambaa ambacho nilikuwa nimekizungusha toka upande mmoja wa bega hadi upande mwingine, na kilemba kilichonikaa vyema kichwani utadhani yule malkia maarufu wa Misri ya kale, Nefititi. Nilikuwa nimevaa mkufu wa lulu nyeupe inayongaa iliyochanganywa na rangi ya dhahabu na midomo yangu nilikuwa nimepakaa lipstick ya rangi nyekundu isiyowiva sana. Nilipokaa na mume wangu macho ya wageni mbalimbali yalikuwa yananiangukia mara kwa mara hasa waliponiona pembeni ya mheshimiwa huyo. Kwa vile mimi si mtu wa kwenda kwenye tafrija zao nyingi za kisiasa ni wachache sana wanaonifahamu kama ni mke wa waziri. Ukiondoa mke wa Rais, na wake za makamu, Waziri Mkuu na hasa mawaziri wote wa juu watumishi wengi wa ngazi za juu na hata wananchi wa kawaida hawanijui. Na kwa vile mimi si mshabiki sana wa siasa basi hata shughuli zangu nyingi hazijulikani kwa wengi. Ni huu mwaka wa uchaguzi tu ndio umenilazimisha kutokea mara kwa mara na Waziri katika mikutano na vikao mbalimbali. Na kila nilipotokea na waziri

basi nilikuwa kama malaika wa heri kwake. Pamoja na mgongano tulionao nyumbani kwetu nimetimiza vyema wajibu wangu kwake kama mke nikimpa kila aina ya mtazamo wa furaha na heri na hata kumshika mkono kwa mapenzi. Bila ya shaka watu wakituona walifikiria angalia *wanavyopendana jamani.* Nilisikia huzuni kidogo nilipofikiria hilo. Ulikuwa ni *unafiki* tu wa daraja la kwanza.

Mlipuko wa sauti za shangwe za nderemo na vifijo, vigelegele na makofi uwanjani hapo uliashiria kuwa hatimaye msafara wa Rais ulikuwa umeingia uwanjani. Karibu kila mtu alisimama na bendera yake mkononi na kuipunga kwa fahari ya Muungano uliozaa Tanzania yetu. Na mimi na bendera yangu ndogonilinyanyuka huko nikipunga kwa furaha kabisa siku hiyo ya Muungano. Bendi ya Jeshi la Polisi ilikuwa inaongoza kwa nyimbo mbalimbali za kizalendo ambazo wananchi walikuwa wanazifuatilia aidha kwa makofi au kwa kufuatisha kwa kugonga miguu yao chini kwa kufuata mahadhi ya muziki.

Msafara wa Rais ulitanguliwa na pikipiki za polisi zipatazo kumi na sita huku wapanda pikipiki wake wakiwa wamevalia nguo nyeupe zinazong'aa, miwani myeusi ya jua, na glovu nyeupe vile vile. Mngurumo wa mapikipiki hayo ya polisi ulijaza uwanja mzima na yakienda taratibu. Kwenye kona ya kulia ambako Rais aliingilia alisimama askari mrefu wa kike wa usalama barabarani ambaye aliyaongoza magari kuelekea mzunguko huo wa uwanja. Msafara huo haukuja moja kwa moja jukwaa kuu bali ulizunguka kuanzia upande wa kulia wa uwanja ambako msafara uliingilia na kufuata mzunguko wa sehemu ya kukimbilia wanariadha kwa mwendo wa taratibu kuelekea mashariki kaskazini na baadaye kugeuzia magharibi ambako ndiko liliko jukwaa kuu.

Rais akiwa amesimama kwenye gari hilo la wazi alikuwa anapunga mikono kwa wananchi waliomshangilia kwa furaha. Ni wazi alifurahia sana shangwe hizo kwani wakati kama huo Rais alionekana yuko kati ya watu wake hasa na tabasamu lake ambalo limekuwa kama alama yake lilikuwa likiupamba uso wake. Pembeni yake alikuwa ni mkuu wa majeshi ambaye alikuwa amejipamba katika ukuu wake wote huku nishani mbalimbali zikining'inia kifuani upande wa kushoto. Generali huyo alikuwa ametilia mavazi yake ya rangi nyekundu angavu, mkono wa kushoto ukiwa umeshikilia ala yenye sime yake ya kijeshi na mkono wake wa kulia ukiwa umeshikilia ukingo wa vyuma wa gari. Mikono yote ilikuwa imefichwa kwenye maglovu ya rangi nyeupe kali. Yeye naye kama alivyokuwa rais alikuwa anatabasamu huku akimrushia Rais maneno mawili matatu. Nilitamani ningekuwa nzi niweze kusikia wanachonong'onezana. Nyuma ya gari la rais kulikuwa na magari ya watu wa usalama, magari ya afya na wapambe wengine wengi tu. Kwenye kila upande wa gari la rais kulikuwa na maafisa wa Usalama wapatao wanne ambao walikuwa wanakimbia taratibu wakilisindikiza hilo gari kwenye uwanja huo. Vijana walikuwa fiti kweli kweli.

Mimi niliangalia hayo yote huku mawazo yangu yakinichezea kama mazingaombwe. Fikra zangu zote zilikuwa kwa Freddy, mjamaika wangu. Japo macho yangu nilikuwa nimeyakodoa uwanjani na mkono wangu na bendera yake vikiwa juu kama nilikuwa nanyosha mkono darasani kujibu swali moyo wangu ulikuwa mbali na uwanja huo. Hisia na vionjo vyangu vyote vilikuwa vinaenda na kurudi; kwa Freddy na uwanjani, kwa mume wangu na nyumbani kwa Freddy. Kwa kadiri nilivyojitahidi kumuweka mbali ya mawazo yangu ndivyo Freddy alivyokuwa ananijia kwa nguvu hadi moyo niliusikia kudunda. Nilijiuliza ilikuwaje kijana huyo ambaye ni wazi nimempita zaidi ya miaka 12 ameweza kuniamsha hisia zangu

za kike namna hiyo sikupata majawabu ya kuridhisha. Katika maisha yangu kweli kabisa sikuwa kuwaza nitakuwa naanguka tena kwa kudondoka kimapenzi kwa kijana kama huyo. Nilijua kwa hakika kwake nimenyong'onyea na kama ndege aliyenaswa mtegoni kwa hakika nilikuwa nimenaswa nikanasika.

Rais alipofika kwenye jukwaa kuu alipokewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam pamoja na viongozi wengine wa kitaifa. Kabla ya kukaa alianza kusalimiana na viongozi wengine wa kitaifa waliokuwa kwenye viti vyao akianza na Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu, Waziri Kiongozi na baadaye marais wa zamani pamoja na viongozi wengine wa juu akiwemo Spika na Jaji Mkuu. Alitupungia mkono na sisi wengine na kuchukua sehemu yake ya kuketi ndipo sherehe zilipoanza rasmi kunoga uwanjani hapo. Vikundi mbalimbali vya burudani vilianza kuburudisha huku uwanja ukisubiri kwa hamu gwaride la Muungano ambalo lilikuwa linaongozwa na Meja mmoja kutoka JWTZ. Vikosi vyetu vyote vya majeshi ya ulinzi na usalama viliwakilishwa vyema uwanjani katika mavazi yao rasmi ya sherehe. Kuanzia wapiganaji wa ardhini, wanamaji, polisi, magereza, KMKM na chipukizi wote walikuwa uwanjani hapo. Wote walionekana kama maua yapendezayo kwenye bustani ya kifalme.

Mume wangu alikuwa alikuwa anapiga soga na waziri mwenzie aliyekuwa upande wake wa kulia na mimi sikutaka kuingilia mambo yao nilikuwa niko katika kufurahia burudani za vikundi vya ngoma za utamaduni. Ngoma ya Kupunga pepo kutoka Zanzibar ilinivutia sana na kujikuta ninacheka mwenyewe kwa hilo wazo la kupungana *pepo*. Wakati uliongojewa na wananchi wengi ulifika pale vijana wa halaiki walipoanza kujipanga katika *formations* mbalimbali.

Wakati vijana wa halaiki wanaanza kuonesha na kufanya vitu vyao mbele ya umati ule mkubwa uliokusanyika kwenye uwanja wa Uhuru nilijikuta ninazama tena kwenye eneo ambalo sikutaka kabisa kuliendea. Sikutaka kufikiria wala kukumbuka kwanini nimefikia siku hiyo na kwa nini nilikuwa niko tayari kwenda nje ya ndoa yangu jioni hiyo ya siku ya Muungano. Nina uhakika wapo ambao wakisikia kisa hiki wangeshangaa imekuwaje mtu kama mimi kufikia kuangukia mikononi mwa mjamaika. Sidhani kama nahitaji kumpa yeyote maelezo ya kujitetea kwani sina deni kwa mtu. Hata hivyo, kwangu mimi mwenyewe nilikuwa nimejishawishi kuwa nitakalofanya lilikuwa ni haki na halali kwangu na ni gharama ya makosa ya mtu mmoja. Mume wangu asingefanya alichofanya kamwe nisingefikia hapo. Machozi yalianza kunilenga nilipoanza kukumbuka chanzo.

Wakati watoto wanaimba wimbo wa "Tanzania Tanzania nchi yenye mali nyingi" mawazo yangu ambayo sikuwa na uwezo wa kuyazuia yalianza kunirudisha miezi saba iliyopita katika siku ile ya machozi, siku ambayo kamwe sitokaa kuisahau. Siku ambayo mume wangu wa ndoa alinitenda ubaya. Siku ile mume wangu aliugeuza moyo wangu uliokuwa unawaka moto wa mapenzi na kuwa moyo ulioganda kama barafu ya uchungu. Kile kisima cha furaha kilichokuwa kikibubujika daima kila nilipomuona kilikuwa kimegeuka dimbwi lenye harufu mbaya ya kinyongo. Nilijitahidi kufuatilia kinachoendelea uwanjani hapo lakini nilishindwa. Nilianza kupotelea taratibu katika giza zito la fikara na mawazo. Nilisikia tu kwa mbali kama mtu aliyeko nje ya ukumbi wa muziki kelele za shangwe na vigelegele toka uwanjani hapo. Kama niliyefungwa kamba na

kuvutwa kama mbuzi machungani nilijikuta napelekwa nisikotaka kwenda. Nilitii.

* * *

Nilikuwa ninasafiri kuelekea Arusha ambako kwenye moja ya mashamba yetu ya shayiri kulitokea ugomvi kati ya wanakijiji na wafanyakazi wetu. Mume wangu alinitaka niende kufuatilia na kujaribu kutatua matatizo hayo na kujaribu kuhakikisha kuwa hayatokei tena hasa akiogopa suala hilo kufumuka kwenye vyombo vya habari. Asubuhi na mapemahiyo ya mwisho wa mwezi Septemba mume wangu pamoja na dereva walinipeleka Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere. Niliingia moja kwa moja chumba cha watu mashuhuri na mume wangu mpenzi aliniaga kwa busu moja motomoto na kuondoka kurudi jijini kuendelea na kazi.

Wakati nasubiri ndege iwe tayari nilianza kujisikia kizunguzungu na tumbo lilianza kuniuma. Mwanzoni nilipuuzia lakini maumivu yalikuwa makali nikaamua kuinuka nilikokuwa nimeketi na kuelekea msalani. Nilipoingia tu kitu cha kwanza nilianza kutapika vyakula vyote nilivyokula asubuhi hiyo. Kidogo nilijisikia nafuu na baada ya kutumia choo kwa karibu dakika kumi na tano niliona tumbo limeachilia kidogo lakini bado nilikuwa na kichefuchefu na kichwa bado kilikuwa kinanigonga kwa mbali. Nilitaka kumpigia simu mume wangu lakini nikaona nifanye uamuzi mimi mwenyewe wa kuahirisha safari. Nilijua siku hiyo asubuhi kulikuwa na mkutano wa kawaida wa baraza la mawaziri ambao huwa unafanyika mara moja kwa wiki. Sikutaka kumsumbua mume wangu kwani sikuwa katika hali mbaya sana. Niliamua kwenda dirisha la Precision Air na kuwaambia kuwa nimeamua kuahirisha safari hiyo hadi baada ya siku mbili hivi. Nikafanya booking mpya.

“Una usafiri mama?” aliniuliza binti aliyekuwa dirishani hapo kwani alinifahamu.

“Nitatumia taxi tu kurudi nyumbani, usijali Haika” nilimjibu.

“Usiwe na wasiwasi mama ngoje tukupatia courtesy ya rentals hapa” alisema na mara moja akapiga simu kwenye ofisi ya magari ya kukodi iliyokuwa uwanjani hapo. Haikuchukua muda kijana nadhifu ambaye alijitambulisha kama ni dereva wa Avis mojawapo ya makampuni ya kukodisha magari kwa wasafiri iliyopo uwanjani hapo. Nilimshukuru Haika na mara moja nilifuatana na dereva yule kuelekea eneo la maegesho ya magari yao ambapo alinifungulia mlango kwenye gari la Toyota Venza la rangi ya kijivu. Nililipenda hilo gari kwani ndiyo lilikuwa limetoka tu kwa mara ya kwanza. Lilipooneshwa mara ya kwanza kwenye maonesho ya Magari ya Kimataifa pale Detroit nilikuwa nimeenda kumtembelea rafiki yangu wa zamani sana ambaye anaishi hapo wakati mume wangu alikuwa Chicago. Nililipenda nilipoliona kule na kuweza kuchukuliwa nalo nilijisikia kama ni test drive. *Nitanunua hili gari* nilijisemea. Toyota Venza ni muunganiko wa gari dogo la sedan na gari kubwa la matumizi ya nyumbani (SUV). Niyajua magari yangu. Baada ya kumpa maelekezo dereva ya kunipeleka nyumbani niliketi kiti cha nyuma kichwa changu kikiwa nimekilaza kwenye kiegezo na kufumba macho yangu kupumzika. Dereva hakuwa mwongeaji kabisa aliniambia tu kuwa nipumzike na akikaribia maeneo ya Kiluvya ataniamsha ili nimpe maelekezo hasa ya kuweza kunifikisha nyumbani.

Nilikuwa bado nina usingizi kwani mume aliukatisha mapemza. Aliniamsha mapema kwa mapenzi motomoto ya asubuhi ambayo bado nilikuwa ninayasikia raha yake. Alijua napenda sana kufanya mapenzi asubuhi na hakunikatili kabisa.

Hivyo muda huo nilijua ningeweza kupumzika kidogo kwani angalau kutoka uwanja wa ndege hadi kufika maeneo ya Ubungo na kushika barabara ya Morogoro kulikuwa na lami nzuri tu. Usingizi ulinichukua kiurahisi tu. Kama dereva aliyebeba maboksi ya mayai dereva wa Avis aliendesha gari kwa uangaliafu mkubwa kuelekea Kiluvya. Hakutaka kuniamsha.

Ilituchukua kama saa moja na nusu kuweza kufika nyumbani kwangu saa tano za mchana. Baada ya walinzi kuchungulia toka ndani na kuona ni mimi walifungua lango la nyumba na dereva aliingiza gari hadi mbele ya nyumba. Palikuwa na ukimya ambao niliutarajia kwani muda huo karibu kila mtu alikuwa katika shughuli mbalimbali. Nilimshukuru dereva na kumpa bakshishi nzuri tu na baada ya yeye kushukuru aligeuza kurudia JNIA na mimi niliingia ndani. Nilikuwa najisikia vizuri kuliko nilivyotoka uwanja wa ndege na nikajisikia vibaya kuahirisha safari hiyo. Niliingia jikoni na kunywa maji baridi kutoka kwenye chupa zilizokuwa kwenye friji. Nilizidi kujisikia vizuri kabisa hivyo sikutaka kulala tena kwani nilipumzika vya kutosha kwenye gari. Niliingia chumbani kwa binti yangu Renata ambaye kama kaka yake alikuwa shuleni asubuhi hiyo. Nilitaka kutumia muda huo kusafisha kidogo na kukipanga vizuri chumba chake. Kwa namna fulani tu nilikuwa najisikia kufanya shughuli za kimama ambazo mara nyingi nilikuwa nimemuachia mtumishi wa nyumbani.

Nilijishughulisha hapa na pale kwenye chumba cha Renata na baada ya muda niliketi kitandani nikifikifiria maisha yangu na mume wangu. Nilijilaza hapo nikiwa na tabasamu na kumshukuru Mungu kwa zawadi nzuri ya maisha aliyonipa ambayo kwa kweli ilikuwa ni neema tupu. Nilimshukuru Mungu kwa kunipa mume mzuri na mwaminifu ambaye alikuwa ananipenda na kunijali na ambaye kwa miaka kumi na nne amekuwa rafiki yangu wa karibu. Waziri alikuwa ni mwanamme pekee niliyemjua. Ni yeye aliyenivunja ubikira wangu na ndiye aliyenifundisha mapenzi na mahaba yote. Mambo ya kutunza nyumba na shughuli za nyumbani nilijifunza kwetu, lakini kwenye mambo ya chumbani, alikuwa kwangu ni profesa mwandamizi. Tulijaliwa kuwapata watoto wetu wawili na kwa hakika walikuwa ndio uhai wangu na wa mume wangu.

Kusema ukweli sijui ni kitu gani kilinifanya nimkubalie yeye kwani wakati ameanza kunitongoza nilikuwa ndio nimeanza kazi tu serikalini na yeye alikuwa ni bosi wangu. Niliapa mapema kabisa katika maisha yangu kuwa sitotoka na mtu yeyote ambaye nafanya naye kazi na hasa akiwa ni bosi wangu. Sikutaka nionekane au nisemwe kwamba nafasi yoyote niliyopita imetokana na kuvua sketi yangu kwa mabosi. Hivyo, licha ya kuwa mchangamfu vijana kazini waliniheshimu sana kwani pamoja na kila gia walizokuwa wanatumia kamwe sikuwa rahisi kunikamata. Nilikuwa nimeazimia kabisa kuwa mwaka huo wa kwanza sitojishughulisha na mambo ya mapenzi kwani nilitaka nizame katika kujifunza hasa kazi yangu.

Kilichonishangaza hata hivyo ni kuwa kati ya vijana na wanaume wote hapo kazini ni mmoja tu ambaye hakuonesha kunitaka wala kuniangalia kwa macho ya matamanio. Angalau hakuniangalia nikamkamata. Alikuwa ni Jonathan Kavishe. Jonathan alikuwa ni bosi mzuri na kila msichana hapo ofisini alikuwa anapenda “kujipitisha pitisha kwake” na ni wazi mimi pia nilimshangaza kwani hata sikumoja sikutaka kujishughulisha na mara zote nilimuita kwa kumuita Bosi au Mr. Kavishe. Nilikuwa *formal* sana kwake. Kwa kadiri miezi ilivyokuwa ikienda pale kazini ndivyo moyo wangu ulivyozidi kutamani Jonathan aseme kitu kwangu. Nilijua alikuwa hajaoa

na alikuwa ni mtu anayependa kazi sana. Hakuna siku ambayo wafanyakazi tuliokuwa chini yake tumewahi kufika ofisini na kumkuta hajawahi kufika isipokuwa kama hayuko mjini. Na vile vile kwa kadiri ninavyokumbuka sijawahi kumuona akitoka kazini kwani karibu mara zote wafanyakazi wote tuliondoka na kumuacha nyuma.

Nilipokuwa nawaza hayo yote singizi ukanipitia. Kama utani vile nilijikuta nimechukuliwa hadi siku ile ambayo bosi alinikaribisha kwake weekend moja. Sijui kwanini nilimkubalia lakini aliniingia kwa gia nzuri sana kwani wala hakuwa na papara. Alianzia mbali sana. Siku moja jioni aliniuliza kama baada ya kazi angependa anipeleke out kwani nami nilichelewa kutoka kazini na akajitolea kunipa ofa ya dinner. Nilijaribu kukataa lakini sikutaka kukataa sana hadi akakata tamaa. Nilimkubalia na akanipeleka kwenye hoteli moja ambayo haikuwa mbali na ofisi zetu maeneo ya Msasani pale Namanga. Wakati huo mimi nilikuwa ninaishi Mikocheni B. Baada ya chakula alinipa lifti hadi nyumbani kwangu ambako bado nilikuwa naishi na wazazi katika mwaka huo wa kwanza kazini.

Kama mara mbili hivi baadaye aliendelea kunitoa dinner na nilianza kumzoea. Hakuna mfanyakazi yeyote aliyejua hilo na hapo ofisini sikutaka kuonesha kwa mtu yeyote kuwa nimeanza kumzoea bosi kwa namna ya urafiki wa karibu. Kwa kweli alikuwa ni mcheshi sana kuliko alivyokuwa anaonekana hapo ofisini. Alikuwa na stori nyingi za seminari alikosoma, jeshini, na alipoenda kusoma huko Uingereza. Nilikuwa nasikia raha sana kumsikiliza na hasa sauti yake ilikuwa ina upole wa aina ya pekee. Sijui hata kama alikuwa ni mtu anayeweza kufoka kwani nilipomfikiria kuwa ananifokea nilijisia kusisimka. Tulikuwa karibu sana na nilijua kabisa kuwa urafiki wetu ulizidi kusogea zaidi zaidi kuwa wa kimapenzi kuliko wa kikazi.

Sasa aliponikaribisha nyumbani kwake nilikuwa natetemeka kwa namna fulani. Alinivunja ubikira kwa hiari yangu mwenyewe na kwa utaratibu ambao siwezi kuusahau. Nilimuambia mapema kabisa kuwa sijawahi kuwa na mwanamme na hakutaka kunipressure lakini alikuwa tayari kusubiri na mimi hadi nitakapokuwa tayari. Sasa siku moja ambayo nilikuwa tayari nilimdokeza na akaniuliza mara kadhaa kama niko sure nataka kufanya mapenzi naye. Nilimhakikishia kuwa kama kungekuwa na mwanamme yeyote ambaye ningempa ubikira wangu basi ilikuwa ni yeye kwani sikuwa tena tayari kumpa mtu mwingine. Na haikuwa sharti la ndoa nilitaka tu yeye awe mwanamme wangu wa kwanza. Na kweli alinifungua uanamke wangu kama zawadi ya malaika mkononi mwake. Siku moja labda nitasimulia.

Baada ya kunizoesha kidogo mapenzi kwa siku kadhaa, nilianza kunogewa na nilianza kuwa na hamu sana ya kufanya mapenzi naye. Sikuweza kumfikiria mtu mwingine yeyote kunigusa namna hiyo kitandani. Nilikuwa kama niliyeonjeshwa asali na nilitaka kubeba mzinga mzima na mti wenyewe pamoja na nyuki! Karibu kila baada ya kazi nilienda kumsubiri kwenye grili moja ya nyamachoma ambako akitoka kazini alinipitia na baada ya kula tulielekea kwake. Kwa kweli alikuwa ana namna ya kufanya mapenzi ambayo nilikuwa sijatarajiia hasa nilipomuangalia ofisini akiwa na suti yake. Aliweza sana kutenganisha mambo ya mapenzi na mambo ya ofisini.

Kwenye ndoto hiyo tamu nilijikuta napelekwa siku ile ambayo sijui ndio niite ilikuwa ni ya kipekee kwani baada ya kufika

pale kwenye grili akitokea kazini hakutaka tukae tule kama ilivyokuwa kawaida. Aliponiona tu alinikumbatia na kunibusu shavuni. Akininong'oneza.

"Mwenzio nina nyege ile mbaya" alisema kitu ambacho sikuwa nimekitarajia wakati huo. Alivyosema hivyo mwili mzima ulinisisimka.

"Jonathan, unanifanya moyo unidunde" nilimnong'oneza.

"Kwa kweli sina hamu ya kula sasa hivi nina hamu na wewe" aliniambia huku akinivuta kuondoka hapo. Niliweza kuona kwenye macho yake tama na kiu. Mikono yake ilikuwa na joto hadi nilidhani ataniunguza.

"Na mimi mpenzi unanitia hamu, Jonathan" nilimjibu kwa sauti ya kulegea. Nilijihisi unyevu wa ghafla.

"Twende bwana" aliniambia. Sikuleta ubishi kwani kwa hamu niliyokuwa nayo ngozi yangu ya mgongoni ilikuwa inacheza cheza kwa kusisimka kama ngozi ya ng'ombe. Tulipoingia ndani ya gari lake sijui alikuwa na mashetani gani. Mkono wake wa kulia ulikuwa umeshikilia steringi lakini mkono wake wa kushoto alikuwa ananichezea mapaja yangu huku akivuta sketi yangu kwenda juu.

"Jon, angalia mbele bwana" nilimhimiza kwa maana macho yake yalikuwa yakikodolea kila sekunde mapaja yangu yaliyonona utadhani Pundamilia wa Serengeti.

"Naangalia" alisema na kuyarudisha macho barabarani. Mkono wake ulibakia kwenye mapaja yangu. Niliyabana mapaja yangu na joto la mkono wake lilinisisimua. Niliyaachia nayeye kwa utundu wake akaupeleka mkono karibu kabisa na malango yangu. Nilijua nikimuachia huyo anaweza kunifanya nionekane mwehu barabarani. Nilimtoa mkono wake kwa masikitiko na kuurudisha kwa nguvu kwenye usukani. Alicheka; na mimi nilicheka. Aliendelea kuendesha gari kuelekea nyumbani kwake maeneo ya Oysterbay.

Niliangalia suruali yake ilivyokuwa imetuna pale na mimi nikashindwa kujizuia.

"Jon, umedinda kweli" nilimuambia na mkono wangu wa kulia nikauweka juu ya suruali yake kumpima urefu wa uanamme wake. Aliguna tu na kuung'ang'ania usukani kama aliyeambiwa akiuchilia basi korodani zake zitapigwa nyundo. Nilimsugua kidogo taratibu juu ya suruali yake. Ingekuwa mahali pengine sijui ningefanya *nini.*

"Tina acha bwana ntapata ajali" alinibembeleza.

"Yaani wewe kunishika isiwe ajali, mimi kukugusa ndio itakuwa ajali" nilisema kwa kicheko cha kejeli. Nilimmimnya kidogo maungo yake hayo. *Laiti angekuwa ameniingia, ingekuta tamu kweli*

"Mguso wako mpenzi unaniumiza naweza kujikuta naegesha gari pembeni nikumalizie hapa hapa maana hata simba hula anapokamatia mawindo" alisema kwa msemo – sijui alitokao nao wapi. Nilijua alikuwa ananitania tu lakini hilo wazo la mtu kuegesha gari kwa vile amezidiwa lilinifanya nimtamani zaidi. Tulipofika nyumbani kwake kwenye mojawapo ya apartments maarufu pale O'bay aliufungua mlango na kunikaribisha ndani. Kigiza kilikuwa kimeanza kuingia ndani ya jiji hili la Bandari Salama. Aliwasha taa za ndani na ile ya nje. Hakutaka kunichelewesha wala kusubiri nijiweke sawa. Alinijia kwa nguvu kama upepo wa dhoruba na kama mnyama aliyekuwa na njaa kali alianza kurarua blauzi yangu. Sijuli alidhania akiamua kufungua zipu mgongoni itamchukua karne, yeye

aliinyofoa kama ukurasa wa daftari ikadondoka. Niliguna. Alianza kunibusu kwa nguvu huku na mimi nikiwa nimelewa mahaba yake nilianza kufungua vifungo vya shati lake. Vidole vyangu vilipogusa ngozi yake nilijisikia umeme wa mapenzi ukinipitia kuanzia utosini hadi kwenye unyayo. Nilinyanyua mguu wa kushoto juu na kuukunja kwa nyuma. Nusura tuangukiane – au nimwangukie.

“Jamani mpenzi” nililalamika

“Ooh Tina” naye alinilalamikia.

“Natamani mate yako mpenzi” aliniambia na bila kusema nilimpa denda. Alizungusha mikono yake mgongoni kwangu na kufungua vipini vya sidiria yangu, sidiria yangu nyeusi ilijiachilia taratibu kati yetu. Tulisogea kwenye makochi maana tulianza vurugu hizo hapo hapo mlangoni mara tu baada ya yeye kuwasha taa. Nilijisikia hamu imezidi. Jonathan alibusu chuchu zangu kama anayetaka kutazifuta kama maembe dodo na alibugia nusu ya nyonyo huku ulimi wake ukichezea chuchu. Nilikuwa nimeanza kufungua mkanda wake kwa haraka utadhani yalikuwa ni mashindano ya kufungua mikanda duniani. Suruali yake ilidondoka sakafuni akawa amebakia na nguo ya ndani tu. Nilimsukuma kwenye kochi.

Tulikuwa tunahema kama wapiga mbio za marathoni. Nilisimama mbele yake nikiwa nimebakia na sketi tu na chupi yangu pamoja na viatu vyangu. Alikuwa amekaa na chupi yake tu. Sijui alikuwa anafikiria nini aliamua kupitisha mikono chini ya sketi na kuanza kuichojoa chupi yangu kwa vurugu. Nilisikia raha. Niliamua mwenyewe kuivuta sketi upande wa kushoto na kuachilia vifungo vyake na zipu. Chupi na sketi vilidondoka kwa wakati mmoja.

Nilipiga magoti mbele yake na bila kuomba kibali nilianza kumvua chupi yake. *Toba yarabi* alikuwa amehamasika na alikuwa tayari kutoa ushirikiano wote uliokuwa unatarajiwa. Kwa kweli wala sikuchelewa na sikutaka kupoteza muda kwani kwa kweli haikuwa ni kufanya mapenzi ya taratibu ilikuwa ni kuondoana kiu na hamu. Nilijipandisha juu yake huku nikijichanua miguu yangu. Kwa mkono wa kushoto nilimuongoza mfalme wa hekalu langu kuingia katika malango yangu. Nilisikia kusisimka hadi kwenye ulimi! Mikono yake aliizingusha kiunoni mwangu na mimi sikumkopesha. Alikuwa amenionjesha utamu na uroda na sikutaka nikinai. Nilianza kumkatikia kwa manung’uniko.

“Ooh Bosi, jamani bosi” nililia huku nikimuendesha kama farasi wa polisi

“Jamani Tina, unakatika vizuri mpenzi” nilitamani kucheka lakini sauti yake ilinifanya nimkolezee!

“Bosi wewe mtamu” nilimuambia kwa sauti ya mahaba. Mwenyewe alipenda sana nikimuita bosi wakati wa kufanya mapenzi. Na yeye akawa ananirudishia mapigo kwa namna hiyo hiyo.

Nilikuwa nalia “bosi bosi” huku akibusu chuchu zangu na kuzinyonya kwa kupokezana. Vidole vyake vilitambaa mgongoni kwangu hadi kwenye matako yangu. Nilishindwa kujizuia. Nilipiga kelele zaidi “bosi bosi, jamani bosi asante bosi, *nakupenda bosi*”

“Na mimi nakupenda *Rehema*” alisema! Nilishtuka baada ya kuniita Rehema! Na mara moja nikashtuka toka usingizini. Lakini sauti za mapenzi zilikuwa bado zinaendelea.

“Bosi nipe zaidi bosi” nilisikia sauti hizo zikitoka kwenye chumba kingine kilichokuwa karibu na cha Renata. Nilishtuka.

“Usiwe na wasiwasi Rehema” niliisikia sauti ya kiume. Mwanzoni sikutaka kuamini kama naifahamu lakini ilikuwa ni sauti niliyoizoea. Sikutaka kuamini. Nilijikusanya kwa haraka nikitetemeka kama kuti kavu lilikokuwa karibu kudondoka. Moyo ulikuwa unanidunda kwa kasi. Nilijaribu kufikicha macho yangu kuona kama nilikuwa bado usingizini. Ilikuwa *live.*

Niliamka kwa haraka na kufungua mlango wa Renata na kuona mlango wa chumba cha mtumishi wetu wa ndani Rehema kikiwa kimefungwa. Sikutaka kubisha hodi. Niliufungua mlango na kama vile ilikuwa sinema Jonathan alikuwa ameitanunua miguu ya Rehema huku akiwa anamuingia kwa raha zake. Nilipofungua ndio alikuwa anafika kileleni. Aligeuka kuniangalia lakini alishindwa kujizuia.

“Tinaaa!” alipiga kelele huku akijiachilia ndani ya binti huyo ambaye naye wakati huo alifungua macho yake! Wote wawili walipigwa na mshangao mkubwa. Jonathan alijichomoa huku binti akiruka pembeni kuchukua nguo zake. Nilishindwa kusema, nilikuwa na ububu wa ghafla. Moyo wangu ulikuwa umechomwa mishale ya moto, nilikuwa kama niliyemwagiwa maji ya baridi ambayo hayakuishia kwenye ngozi juu tu bali yalizama hadi kwenye mifupa yangu. Niliinamisha kichwa kidogo upande na kumuuangalia mume wangu kwa macho ya masikitiko ambayo hata shetani angeweza kuona masikitiko. Sikuamini kwamba alikuwa anafurahia mahaba ya mtumishi wetu wa nyumbani ambaye mara zote alikuwa akimuita “baba”. Alikuwa ni binti ambaye amekuwa akitusaidia hapo nyumbani kwa karibu miaka sita tangu akiwa na miaka kumi nane hivi. Nilimchukulia kama sehemu ya familia na hata kumpatia elimu ya sekondari ili hatimaye aweze kujitegemea. Sikutarajia kuwa alikuwa ni mke mwenzangu. Yaani msomi, na mtu mwenye heshima zake katika jamii alikuwa mikononi mwa mtumishi wake. *Astaghafillulah!*

Nilifunga mlango; machozi yalianza kunidondoka nikielekea kwa haraka ghorofani chumbani. Akili zangu zilikuwa zimeniruka.

“Jamani Clementina samahani, ni shetani tu *kanipitia*” nilimsikia mume wangu akinikimbilia nyuma yangu. Sikumjibu.

“Tina fadhali nisamehe yule binti ndiye alinichokoza” aliendelea. Sikumjibu.

Niliingia chumbani, machozi yakinidondoka. Nilienda moja kwa moja kwenye kabati la nguo, nilichukua sanduku na kuanza kupanga vitu mbalimbali.

“Baba Renata, yaani unaisaliti ndoa yako namna hii” nilifanikiwa kusema sauti yangu ikikatika katika kwa kwikwi. Ilikuwa imefika majira ya saa nane za mchana. Sijui aliingia saa ngapi kutoka ofisini na sikutaka kujua mahusiano yao yamekuwa ya muda gani. Nilichojua ni kuwa sikutaka kuwa karibu naye hapo.

“Jamani, mpenzi nisamehe kweli naapa *sitorudia* tena” alisema. Nilijiambia moyoni kuwa na wala sitokupa nafasi ya kurudia tena. Nilianza kufungasha. Nilihitaji kwenda mahali ambapo ningeweza kutuliza kichwa changu. Nilimuambia naenda kwa kwa kakangu anayeishi maeneo ya Makongo. Nilimuambia sitaki kumuona wala kuzungumza naye. Nilichukua ufunguo wa gari na kijisanduku changu.

“Mama samahani” Rehema alikuwa analia amepiga magoti sebuleni mbali nami. Sikutaka kumsemesha. Alikuwa ni mtoto wa kike, kosa lilikuwa ni la *mume* wangu.

“Malizana na *mume* wako” nilimuambia nikifungua mlango na kutoka kuelekea kwenye gereji. Nilichukua Toyota yangu na kuondoka hapo. Nilikuwa nalia kama niliyefiwa. Akili yangu ilikuwa inanizunguka kama pia kichwani mwangu. Niliangalia mbingu na kuona kama imekula njama dhidi yangu. Niliiona hiyo nyumba yetu kama jumba la wafu. Nilijisikia kupachukia. Nilimchukia Jonathan. Sikuamini mtu niliyempa moyo wangu wote, tama yangu, hisia yangu, na vionjo vyangu vyote hakuweza kutosheka nami. Hakuna siku aliyotaka penzi langu nilimnyima na kila alipotaka nilimpa hadi cha ziada. Kwake nilitosheka; ilikuwaje kwangu *hakutosheka*.

Nilikaa kwa kaka kwa karibu wiki moja. Jonathan alijaribu kupiga simu kuzungumza na kaka yangu ambaye alikuwa ananilinda sana. Alimhakikishia kuwa bado nina hasira na ampe muda anishawishi niweze kurudi nyumbani. Baada ya wiki moja nilianza kutulia. Niliwamiss watoto wangu, na niliimiss nyumba yangu. Mama alikuja kutoka Arusha ambako walikuwa wamehamia baada ya kustaafu. Mama alinikalisha chini na kunizungumzisha hekima. Alinisisitizia juu ya uzito na majaribu ya ndoa. Alinihoji kama nilikuwa tayari kumuchia mtumishi nyuma na mume. Alinihoji kama ndani ya moyo wangu nisingeweza kumsamehe mtu niliyempenda na kujitoa kwake. Nililia mbele za mama kama mtoto. Wifi yangu na kaka nao walinikalisha chini. Kwa kweli niliingia kwenye ndoa nikiwa na mawazo ya pepo tu; sikutegemea maumivu ya usaliti. Baada ya muda nilikubali kurudi. Mume wangu alikuja kunichukua.

Hakuna siku nilimuonea huruma kama siku hiyo kwani pale nyumbani kwa kaka palikuwa kama hekalu la wafalme wa mbinguni. Aliingia kwa machozi na kwa kutetemeka. Hakutaka kusema lolote. Kaka alimfokea (kaka yangu aliwahi kuwa mwanamasumbwi maarufu nchini) na mama alimuita pembeni na kumkanya kwa lugha kali hadi nikahuzunika maana alikuwa anaitikia “ndio mama”. Jonathan alikuwa kama mtoto mdogo. Mwisho nilimuonea huruma nikaamua tu kumuambia anichukue tuondoke. Niliamua kumuokoa kwani ningeendelea kumuachia hapo angeumizwa kweli na famili yangu. Hatukuzungumza kwenye gari. Alikuwa bado ni mume wangu. Niliwaza *talaka.*

Ndio ulikuwa mwanzo wa umbali wetu. Ulikuwa ni mwanzo wa machungu yangu. Kwani baadaye yule binti wa ndani ambaye tulikwisha mtimua toka siku ile alikuja na kudai ana mimba ambayo alisema ni ya mume wangu. Tulitunza siri hizo toka kwa watoto wetu na hata kwa familia. Nilikuja kugundua tena baadaye kuwa mara kadhaa mume wangu ameenda kumuona yule binti huko Mbagala japo kwa kujificha akidai ati kama ni mtoto wake kweli ni lazima amtunze. Na hata alipoamua kukiri kuvunja kabisa uhusiano na Rehema niliamua kumuwekea ngumu hadi mimi nitakapoamua kumsamehe toka moyoni. Nyumbani palikuwa na vita baridi.

Niliamua siku ile pale barabarani nilipogongana na mjamaika kuwa na mimi katika maisha yangu nifafanya kitu ambacho kitanipa raha mimi mwenyewe na nisingekaa kukijutia. Nilikuwa nimeamua kuwa ili nimsamehe kweli ni lazima na mimi nimfanye ajue kuwa nimekuwa mtu mzima na bado naweza kutamanisha mtu na kumpata ninayemtaka. Sikutaka kuwa mtumwa wa mapenzi yake. *I too had options.*

* * *

“Hima Hima! Tanzania!!”

“Hima hima! Tanzania!!” vikosi vya majeshi ya ulinzi na usalama viliitikia wakati vinakula kiapo cha utii kwa Katiba na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Ndipo akili yangu ilirudishwa uwanjani hapo. Sikumbuki mambo ya kina Mjomba wala gwaride. Sikumbuki gwaride lilikuwa zuri kiasi gani. Lakini nilipoangaza macho uwanjani hapo sura za watu wote zilikuwa zinaonesha uchangamfu na kuridhika. Na mimi niliendelea kupepea bendera yangu ya taifa. Mume wangu naye alikuwa amezama katika kuangalia yanayoendelea uwanjani hapo huku akiendelea kupiga soga na waziri mwenzie.

Na ndipo mawazo yangu yakarudi kwa Mjamaika wangu. Nilitamani angekuwa pembeni yangu uwanjani hapo. Kama ile tamaa yangu kwa mume wangu miaka ya mwanzo ya urafiki na ndoa nivyo nilivyomtamani Freddy. Nilitamani mtu mmoja atamke tu “sherehe zimekwisha” ili nitimke kwenda moja kwa moja kwa Freddy. Hata hivyo, sikuwa na ujanja. Nilisubiri kama wengine na baada ya sherehe uwanjani hapo kwisha na sisi tuliondoka. Tulirudi na mume wangu nyumbani na yeye hakukaa sana nyumbani kwani alikuwa anafanya haraka kujiandaa kurudi tena Ofisini kidogo halafu kwenda Ikulu kwenye sherehe ya Rais na mabalozi na viongozi wengine wa kitaifa kwenye halfa ya chakula cha jioni. Aliniacha nyumbani kujiandaa kwenda kwenye harusi a.k.a Muungano na Freddy.

Nilipoingia bafuni kuoga majira ya saa kumi na mbili nilikuwa nimepumzika vya kutosha na nilikuwa tayari kwenda kukutana na Freddy wangu. Nilianza kujipambana kimwanamke hasa. Nilikuwa nimenyoa kila sehemu ya mwili wangu na kurudia tena jioni hiyo. Nilipomaliza kuvaa nilijipulizia manukato ya Secret of the Desert ambayo niliyanunua kama mwezi mmoja nyuma kutoka pale Cairo Misri kwenye duka la Cleopatra Palace Perfumes ambalo ni maarufu sana kwa manukato. Niliambiwa na rafiki yangu tuliyekuwa tunatoka pamoja shopping Dubai kuwa manukato hayo yanadaiwa kuongeza *mahashhash* na *mashamsham* ya mapenzi. Nilijiangalia kwenye kioo nikajipenda mwenyewe. Saa moja kasoro hivi niliingia kwenye Mercedes yangu na kuondoka kwenda kukutana na Freddy.

Mawazoni mwangu wimbo ulikuwa unasikika “Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote”.

Msafara ulianza wa siku ya kukumbukwa. Uwanja wa kitandani.

^ ^ ^



Hadithi mpya ya "Uso kwa Uso na Kamanda" itakujia baada ya wiki chache zijazo. Itapatikana kwa mchango kidogo pamoja na kisa kingine cha kusisimua vyote vikipatikana kwa barua pepe TU. Itaweza kupatikana kwa mchango kidogo kwenda JamiiForums ambapo kiasi kitabakia kusaidia JF. Utaweza kulipia kwa njia ya simu – vocha na kwa walio nje ya nchi wataweza kujipatia kisa hiki kwa njia ya paypal na kazi za kibenki. Ili uwe wa kwanza kujulishwa kuwa kisa hiki kiko tayari na kuweza kujipatia nakala yako jiunga nami kwenye Facebook - "Mzee Mwanakijiji" au niandikie mwanakijiji@jamiiforums.com kutaka uwe miongoni mwa watakaojulishwa utaratibu wa kukipata kisa hiki kipya na kinachokwenda na wakati. Kama unafikiri umewahi kusoma hadithi za kusisimua basi hujakutana na "Kamanda"!

Kwa sasa ni mchango wa 7.99USD au 8,000Tshs kwa mtu mmoja unaangaliwa.

MMM - Mtunzi